



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA NKASI



Unapojibu tafadhali taja.

Kumb. Na. Nks/DC/M.10/VOL IV/52

02.03.2026

TANGAZOLA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi anakaribisha maombi ya nafasi arobaini (40) za ajira ya ukusanyaji wa mapato kwa Watanzania wote wenye sifa.

SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe na ufaulu wa elimu ya kidato cha nne na kuendelea.
- Awe na ujuzi wa kutumia simu janja.
- Awe mwaminifu, mtii na mwenye nidhamu kazini.

A. MAJUKUMU

- Kukusanya mapato kutoka vyanzo mbalimbali vya Halmashauri.
- Kuwasilisha fedha benki zinazokusanywa kila siku

B. MALIPO/MSHAHARA

Mkusanyaji wa mapato atalipwa asilimia tano (5%) ya mapato aliyokusanya, malipo yatatolewa kila mwezi.

C. MUDA WA MKATABA

Muda wa mkataba wa ajira ni miezi sita (6). Aidha, wokusanyaji watakaokusanya vizuri watafikiriwa kuongezewa muda wa mkataba.

D. MASHARTI KWA WAOMBAJI

- Awe raia wa Tanzania, awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Muombaji aambatishe maelezo yake binafsi (CV), anuani kamili.
- Maombi yalitishwe kwa Mwenyekiti au Mtendaji wa Kijiji anachoishi muombaji.
- Muombaji aambatishe nakala za vyeti vya elimu, cheti cha kuzaliwa, nakala ya kitambulisho cha taifa(NIDA).
- Picha moja ibandikwe kwenye barua ya mombi.
- Muombaji atakayewasilisha taarifa za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria.
- Kwa Muombaji ambae ana kesi mahakamani au kuhukumiwa zaida ya miezi sita(6) haruhusiwi kuomba kazi hii.
- Testimonials na provision statement result, transcript, hati ya matokeo ya kidato cha nne **havitakubalika**.

E. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI YA KAZI

Iwapo unaamini unaweza kuthibitisha wazi uwezo wako wa kukidhi vigezo vilivyotajwa hapo juu, tafadhali wasilisha barua yako ya maombi ya kazi kupitia anuani:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI,
BARABARA YA IKULU,
S.L.P 02,
NAMANYERE - NKASI.

F. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 16/03/2026

Imetolewa na;
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

Ofisi ya Mkurugenzi: 2 Barabara ya Ikulu, S.L.P. 02 Namanyere Nkasi. Simu: +255 025 282 0006.